

**MUHULA WA PILI 2023**  
**KISWAHILI**  
**KARATASI YA KWANZA (102/1)**  
**KIDATO CHA NNE (4)**  
**MUDA: SAA 2 ½**

**MWONGOZO**

- 1 Barua iwe rasmi  
 Barua ichukue muundo wa barua rasmi.  
 Mwanafunzi aeleze vile alivyopata habari/ gazeti  
 anwani mbili, za mwandishi na mwandikiwa  
 Wasifukazi
- Mwanafunzi azingatie maelezo ya kibinafsi  
 Mf. Jina, Anwani, Umri n.k.
- Kiwango cha elimu – kuanzia kiwango cha juu hadi cha chini
- Tajriba yake
- Uraibu
- Warejelewa

**kumb:** mwanafunzi aandike barua rasmi kwanza mpaka amalize kwa kutia sahihi kisha aambatanishe wasifukazi.

**SWALI LA 2.**

Mtahiniwa aunge mkono kauli hii kwa hoja zifuatazo:

- (i) Ongezeko la idadi ya watu.
- (ii) Kulima kandoni mwa mito.
- (iii) Ufisadi – kwa mfano wizi wa mbolea,
- (iv) Sera mbaya za serikali kama vile kugawa mashamba madogo madogo
- (v) Vita vya kikabila ambapo baadhi ya jamii hutoroshwa na kuacha mashamba.
- (vi) Kutumia njia za ukulima zilizopitwa na wakati kwa mfano kutegemea mvua.
- (vii) Kutumia mbegu ambazo hazijafanyiwa utafiti.
- (viii) Kupuuza vyakula vinavyostahimili kiangazi kama mbaazi.
- (ix) Vijana kuhamia mijini na kuwaacha wazee mashambani
- (x) Kilimo/zaraa kudharauliwa na wengi.
- (xi) Kukata miti
- (xii) Kutumia vifao duni/si vya kisasa katika ukulima k.v kiserema.

Kumbuka: Mtahiniwa aunge kauli hii mkono. Akipinga, amepotoka.

**SWALI LA 3.**

Watu wanaofanya kazi pamoja hawakosi kutofautiana / kuwa na mitazamo tofauti

Mambo Muhimu

- (i) Si lazima mwanafunzi aeleze maana ya methali.
- (ii) Lazima atoe kisa kinachoafiki maana ya methali.
- (iii) Lazima pande zote mbili za methali zishughulikiwe. Akishughulikia upande mmoja asipate zaidi ya (C+) (alama 10)
- (iv) Ikiwa kisa hakiafiki maana ya methali, amejitungia swali na atuzwe D- (alama 2)

#### SWALI LA 4

-Mtahiniwa atunge kisa kinachoonyesha unafiki

1. Lazima mtahiniwa amalizie kwa kifungo alichopewa. Akiongeza maneno zaidi, amejitungia swali, atuzwe D- (alama 2)
2. Akianza kwa maneno aliyopewa au kuyatumia katikati, amejitungia swali, atuzwe D-



